# KIBURI

0729 200 777

Sammy Ikua




Copyright © 2017 <Laikipia Campus>
All Rights Reserved


we-we u - li-ye ma-ji-vu ma-vu-mbi-ni u-li-to-ka na ma-vu-mbi-ni
u - li-ye ma-ji-vu u-li-to-ka na ma-vu-mbi-ni
u - li-ye ma-ji-vu ma-vu-mbi-ni u-li-to-ka na ma-vu-mbi-ni
u - li-ye ma-ji-vu u-li-to-ka ma-vu-mbi-ni
1.
2.
u - ta - ru - di mbo - na u di
u - ta - ru - di u di
u - ta - ru - di u di
u - ta - ru - di u - di
1.U-na-ji - vu-na kwa-mba u-na-yo ma-li nyi-ngi u-na-dhu-lu-mu wa-nyo-nge




---

## KIBURI (BY SAMMY IKUA)

**Kiburi ni chukizo kwa Mungu na kwa Binadamu, na kwa wote wawili udhalimu ni chukizo. X2**

**{Mbona unafanya kiburi, wewe uliye mavumbi,**

**Mbona unafanya kiburi wewe uliye majivu} x2**

1. Unajiona kwamba unayo mali nyingi, unadhurumu wanyonge kwa kuwanyima haki, kumbuka mali hiyo imetoka kwa Mungu.

2. Unajifanya kwamba unazo shughuli nyingi, unakosa muda hata wa kwenda kanisani, kumbuka maisha yako ni mali yake Mungu.

3. Mungu anawakweza wale walio wanyonge, anawaenzi wale walio wanyenyekevu, na wenye kiburi anawashusha wote.

4. Tuvitumie vyote tulivyopewa na Mungu, tuvitumie katika kumtukuza Bwana, kwa maana yeye atatujalia mema yake